UHURU UK 6, TAREHE 22.02.2021

# CCM yacharuka migogoro ya wakulima, wafugaji

Katika kipindi cha Papo kwa Papo cha mwishoni mwa wiki iliyopita, ambacho ni sehemu ya 12, tangu kianze kurushwa mwanzoni mwa mwaka huu, Polepole alitumia muda mrefu kupokea simu za wananchi na kuwasilisha kero zao papo kwa papo kwa watendaji wa serikali ili kuzipatia utatuzi.

**NA WILLIAM SHECHAMBO**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeeleza kusikitishwa kwake na uwepo wa migogoro ya rasilimali ardhi baina ya wakulima na wafugaji kwenye baadhi ya maeneo, licha ya juhudi mbalimbali za serikali kuondoa hali hiyo.

Hatua hiyo imekuja baada ya wananchi kadhaa kutoka mkoa wa Pwani na Tanga, kutoa taarifa ya migogoro hiyo kwenye kipindi cha Papo kwa Papo, kinachofuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025.

Kipindi hicho kinaratibiwa na Idara ya Itikadi na Uenezi, kupitia kwa Katibu wa NEC, Humphrey Polepole na kurushwa kwenye vyombo kadhaa vya habari na mitandao ya kijamii, kila Jumamosi, saa 3.00 usiku hadi saa 5.00 usiku.

Akizungumza kwenye kipindi hicho, mwishoni mwa wiki iliyopita, Polepole alisema amepokea malalamiko ya wakulima dhidi ya wafugaji kutoka Kijiji cha Mswaki, wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga na Bagamoyo mkoani Pwani.

Polepole, alisema kwenye lalamiko la kwanza, wakulima wa kijiji cha Mswaki, wilayani Kilindi, wamedai kuonewa mara kadhaa na wafugaji wanaoingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kuharibu mazao.

Mara kadhaa, alisema serikali kupitia kwa Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO), imeelekeza wafugaji kutumia fursa ya uwepo wa kampuni hiyo ya umma, kulisha mifugo yao kwenye maeneo rasmi yaliyotengwa, lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua.

Hata hivyo, alimpigia simu Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Sauda Mtondoo, kumweleza juu ya mgogoro huo, ambapo DC huyo alisema hana taarifa nao, lakini akaahidi kuufuatilia ili kupata suluhu.

"Sijalipata hilo tukio, ila nitalifuatilia kwa sababu awali tulikuwa na tatizo la mgogoro wa ardhi kati ya wakulima na wafugaji kuhusu kufungwa kwa njia za mapitio ya mifugo kwenda josho.

"Tumeshatoa maagizo kwa viongozi wa vijiji wafungue hizo njia, ili wafugaji wapitishe mifugo yao, jambo litakaloepusha mifugo kuingia kwenye mashamba ya watu," alisema.



MKUU wa wilaya ya Bagamoyo, Zainab Kawawa

Kadhalika, Polepole alisema tukio lingine lililohusisha mvutano wa wafugaji na wakulima ni katika eneo la Ruvu Kitonga, wilayani Bagamoyo, ambapo licha ya serikali ya mkoa na wilaya kufuatilia utatuzi wake kwa muda sasa, bado hali siyo shwari.

Alisema kipindi kilichopita, wakulima kadhaa kutoka eneo hilo waliwasilisha malalamiko yao Ofisi Ndogo ya CCM ya Makao Makuu, Lumumba, Dar es Salaam, kuhusu mgogoro huo.

Polepole, alisema Chama kilivyopokea malalamiko hayo, kiliwasilisha ofisi ya mkoa husika (Pwani), ambayo pia ilishusha maagizo ngazi ya wilaya (Bagamoyo), kisha polisi, lakini hadi wiki iliyopita, bado hali ilikuwa si nzuri.

Ili kufuatilia utekelezaji wake, Polepole alimpigia simu Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ambaye alisema wiki hii ana ratiba ya kufanya ziara ya kikazi wilayani Bagamoyo, eneo la Chamapweza na Ruvu Kitonga.

Kwa upande wake, Mkuu wa wilaya ya Bagamoyo, Zainab Kawawa, alisema eneo hilo limekuwa na mvutano wa miaka miwili sasa, kuanzia mwaka 2019, ambapo mwisho pande zote mbili zilifikishana mahakamani.

"Ni miaka miwili sasa, wafugaji waliingia kwenye maeneo ya wakulima, shauri likafikishwa mahakamani (Mahakama ya Wilaya), lakini hukumu ikawanyima haki wakulima, nahisi ndipo wakaamua kuja huko kulalamika," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya, alisema kwa kuwa Mkuu wa Mkoa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Mahakama ya Mkoa, alimuomba licha ya uamuzi wa mahakama, wafugaji waamriwe kulipa fidia wakulima kutokana na uharibifu uliofanyika kwenye mashamba ya wakulima.

Zainab, alisema anaendelea kufuatilia mgogoro huo kwa ukaribu na kuwataka wananchi kuwa wavumilivu wakati ambao serikali inafanya kila juhudi kumaliza mgogoro huo na kutoa haki inayostahili.

Kutokana na kauli hizo za watendaji wa mkoa na wilaya,



MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo

Polepole, alisema ufuatiliaji wa mgogoro huo siyo kuingilia mhimili wa mahakama, bali kujadili na kupata majibu ya shaka iliyopo kwenye upande mmoja uliodnewa na upande mwingine.

Alipendekeza hukumu iliyotolewa na mahakama ya wilaya dhidi ya wakulima, kuangaliwa kwa ukaribu na kamati ya maadili ya mahakama ya mkoa, ili yule aliyekiuka maadili kwenye hukumu hiyo, sheria ishike mkondo wake.

**MKUTANO NA WANANCHI 300**

Wakati huohuo, Polepole alisema juzi, kwa kutekeleza maagizo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka huu, fungu la 251, fungu dogo (e), alikutana na wananchi zaidi ya 300 nje ya Ofisi ya Chama Lumumba ili kusikiliza, kutatua kero za wananchi.

Alisema mkutano huo ulifanyika kuanzia saa 10.00 alasiri hadi saa 1.30 asubuhi, utaratibu unaofanywa pia na viongozi wote wa juu wa Chama kwenye ofisi ya Makao makuu Dodoma na Lumumba, Dar es Salaam.

Katika kipindi cha Papo kwa Papo cha mwishoni mwa wiki iliyopita, ambacho ni sehemu ya 12, tangu kianze kurushwa mwanzoni mwa mwaka huu, Polepole alitumia muda mrefu kupokea simu za wananchi na kuwasilisha kero zao papo kwa papo kwa watendaji wa serikali ili kuzipatia utatuzi.

**MALALAMIKO**

**WAKULIMA WALIA KUONEWA**

Akizungumza kwenye kipindi hicho, mwishoni mwa wiki iliyopita, Polepole alisema amepokea malalamiko ya wakulima dhidi ya wafugaji kutoka Kijiji cha Mswaki, wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga na Bagamoyo mkoani Pwani.



MKUU wa Wilaya ya Kilindi, Sauda Mtondoo

Scanned with CamScanner

# Kulisha mifugo mashambani sasa kukaa mahabusu siku 10

**Na Richard Makore,** MAGU

MKUU wa Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, Salum Kali, ametangaza kuwakamata na kuwaweka mahabusu kwa siku 10 mfululizo kabla ya kuwafikisha mahakamani wafugaji wakorofi wanaolisha mifugo yao kwa makusudi kwenye mashamba ya wakulima. Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika kijiji cha Nyashimba katika Kata ya Nyigogo, wilayani Magu alipokutana na wafugaji na wakulima.

Alisema mfugaji atakayekamatwa amelisha mifugo yake katika shamba la mkulima afikishwe kwake na ataagiza awekwe mahabusu kwa siku 10 mfululizo kabla ya kufikishwa mahakamani ili iwe fundisho.

Akizungumza na wakulima na wafugaji katika kijiji hicho, Kali alisema serikali inatakiwa kushughulikia kero ya madawati, barabara, zahanati, huduma za maji pamoja na umeme, lakini siyo kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji.

Alisema kuanzia sasa mifugo itakayokamatwa shambani inauzwa na fedha hizo zitatumika kujenga zahanati, madawati na huduma za afya. Aidha, aliwataka wakulima kuacha njia ya upana wa mita 15 ili kupitisha mifugo badala ya kulima eneo lote na kusababisha migogoro na wafugaji.

"Wote nyinyi ni ndugu, mpendane, mheshimiane kwa sababu mnaishi pamoja mnapakuliana mboga na kuombana moto, hivyo lazima muishi kwa upendo na kuacha migogoro," alisema Kali

Kali alisema ni aibu kwa uongozi ngazi ya wilaya kwenda kushughulikia masuala ya migogoro ya wakulima na wafugaji vijijini badala ya kufanya mambo makubwa ambayo yataisaidia jamii kupiga hatua.

Aidha, aliwataka wenyeviti wa vijiji na vitongoji kumaliza migogoro ya wafugaji na wakulima inayotokea katika maeneo yao badala ya kusubiri viongozi wa juu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza, Hondola Mpandalume, aliwaonya watendaji wa kata na vijiji wanaoshindwa kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji.

Scanned with CamScanner

# Maofisa watajwa tuhuma kuhusu nyama isiyokidhi ubora

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

■■UUZAJI wa nyama usiokuwa na vigezo vya ubora umehusishwa na baadhi ya maofisa nyama walioko kwenye kitengo cha ukaguzi wa nyam.

Hayo yamebainishwa jijini Dodoma na Uchunguzi wa Majira uliofanywa kwa zaidi ya wiki moja katika maeneo mbalimbali ya bishara hiyo kuanzia machinjioni, kwenye mabucha hata kwa wauzaji wa vyakula hasa mamalishe.

Uchuguzi huo ilitokana kuwepo taarifa za nyama zisizo na ubora kuuzwa, hasa mama ntilie ambao kwa upande mwingine wanapata wateja wengi kwa kutokana na kuuza chakula kwa gharama nafuu.

Baadhi ya mambo yaliyobainika ni kutokuwepo usimamizi mzuri wa ukaguzi wa nyama, hata inapobainika nyama isiyotakiwa kufika kwa walaji badala ya kutetekezwa, inatoroshwa na kuuzwa kiholela, huku wateja wakubwa wakiwa ni mama lishe na kwenye vilabu za pombe za kienyeji.

Vilevile, imebainika kuwa baadhi ya wadau wa nyama choma, wanaouza nyama ya vipande, baadhiyao wamekuwa wakiuza nyama isiyokuwa na ubora na mauzo hayo hufanyika zaidi kwenye maeneo yanayouza pombe za kienyeji.

Mfanyabishara mmoja wa nyama choma anayefanya biashara hiyo maeneo ya jirani na Hospitali Kuu ya Rufaa (jina linahifadhiwa) alikiri kuwepo nyama hizo, huku akisema yeye hausiki.

Alisema si rahisi kwa nyama isiyokuwa na ubora kutekefezwa badala yake zitafanywa kila mbunu ili iingizwe sokoni.

Naye afisa mmoja wa idara ya nyama, ambaye hakata kutajwa majina, aliliirusha sakata hiyo kwa bodi ya nyama na kuitaka kusimamia ubora wa nyama tangu utayarishaji wake, kuisimamia vizuri na kudhibiti ukataji wake usiokuwa sahihi kama vile kutumiwa magogo, kunin'giniza nyama kwa wa kutumia nondo.

Naye Msajili wa Baraza la Veterinari, Dkt. Bedan alishauri kuwepo na hali ya ubadilishwaji wa maofisa wa afya.

Alisema wakidumu muda mrefu katika eneo moja kunawafanya kufanya kazi kwa mazoea.

Scanned with CamScanner

# Walengwa TASAF waomba elimu ya ufugaji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WALENGWA wa mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), mkoani Shinyanga, wameomba kupatiwa elimu ya ufungaji mifugo ili kuepukana na vifo.

Walibainisha hayo kwa nyakati tofauti wakati wa ziara ya maofisa wa TASAF walipozunguka Mkoa

ya walengwa katika kujikwamua kiuchumi.

Mmoja wa walengwa hao kutoka kijiji cha Iselamagazi Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Fotunata Mosha, alisema baada ya kupata fedha za TASAF mwaka 2015, alianza na mradi wa kununua kuku, lakini kutokana na ukosefu wa elimu ya ufugaji, walianza kufa kwa magonjwa. "Tunaomba maofisa mifugo watupatie elimu ya ufugaji bora

na hata kondoo zangu hizi 26 sijui namna ya kuzitunza na hofu na wao kufa nikarudi umaskini," alisema Mosha.

Naye Wande Shija ambaye ni mlengwa wa TASAF kutoka kijiji cha Mwadui wilayani Kishapu, alisema alikuwa na kuku 10 lakini walikufa kutokana na ugonjwa.

Ofisa mifugo wa Iselamagazi wilayani Shinyanga, Justine Mkulasi, alikiri kuwapo na tatizo hilo la

kutembelea walengwa wa TASAF kwenye kaya zao kutoa elimu ya ufugaji, na kubainisha changamoto inayowakabili ni ukosefu wa usafiri, pamoja na kutopata taarifa za ugonjwa wa mifugo hiyo kutoka kwa wahusika.

Kwa upande wake, Mkuu wa kitengo cha mawasiliano kutoka TASAF makao makuu, Zuhura Mdungi, alisema moja ya changamoto ambayo inapaswa kufanyiwa

kazi ni utoaji wa elimu ya ufugaji na kilimo kwa walengwa hao.

Mratibu wa TASAF wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Rehema Edsoni, alisema changamoto hiyo ya utoaji elimu ya ufugaji na kilimo kwa walengwa wa TASAF itafanyiwa kazi, huku akibainisha tangu 2015 hadi 2020, wameshatoa kiasi cha Sh. bilioni 6.7 kwa walengwa 5, 125, na sasa wapo kwenye utoaji wa fedha hizo kwa awamu nyingine.

Scanned with CamScanner